

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA KILIMANJARO

Anwani ya Simu: "REGCOM KILIMANJARO"

Simu Na: 027-2754236/7

Nukushi Na. 027-2753248/027-2751381

Barua pepe E-mail: ras@kilimanjaro.go.tz

ras.kilimanjaro@tamisemi.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

S.L.P 3070.

MOSHI.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mnamo tarehe 10/11/2019 majira ya saa 8:30 (nane na nusu) usiku, Mhe. Dkt. Anna Mghwira Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro amepokea taarifa ya kuungua moto kwa jengo la ofisi ya Kata ya Soweto, Manispaa ya Moshi, ambapo ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata hiyo iliungua na kusababisha baadhi ya nyaraka na samani za ofisi hiyo kuteketea.

Harufu ya Moshi iliyochanganyika na mafuta ya petroli ilimshitua mkazi mmoja anaeyeishi jirani na ofisi hiyo ambaye alichungulia nje na kuona jengo la ofisi ya kata likiungua moto.

Jirani huyo aliwaamsha majirani wengine na kutoa taarifa kwa jeshi la polisi. Baada ya kupokea taarifa hiyo kikosi cha doria kata ya Soweto kwa kushirikiana na wananchi walifanikiwa kuuzima moto huo.

Kwa mujibu wa uchunguzi wa awali, moto huo uliwashwa kwa makusudi kupitia madirisha ya mbele ya jengo hilo ambayo yanaonesha kuwa yalimwagiwa mafuta ya petroli na kuwashwa kwa kiberiti.

Wahalifu hao walitelekeza kiberiti ambacho kimeonekana kikiwa na njiti pamoja na msokoto wa bangi.

Moto huo umeunguza sehemu ndogo ya jengo na nyaraka zote zilizokuwa karibu na madirisha. Miongoni mwa nyaraka hizo ni pamoja na taarifa mbalimbali za chanjo, machapisho na makabrasha ya afya.

Kufuatia tukio hilo Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro anapenda kuwataka wananchi wote wa Kata ya Soweto kuwa watulivu kwani suala hili linashughulikiwa na lipo mikononi mwa vyombo vya ulinzi na usalama.


Aidha, Mhe. Mkuu wa Mkoa anayakumbusha makundi yote katika jamii hususani vijana kujiepusha kabisa na vitendo vya kihalifu wakati wowote

mahali popote ndani ya mkoa wa Kilimanjaro, na wanapoona viashira vyovyote vya uhalifu wasisite kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama.

Hadi kufikia sasa serikali imeshachukua hatua za awali ikiwa ni pamoja na kuwakamata watuhumiwa wa uhalifu huo.

Mhe. Mkuu wa Mkoa ameviagiza vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuwa macho na vitendo vyote vya uhalifu vyenye nia ya kuvuruga amani na usalama na kuwashughulikia wahalifu wote kwa mujibu wa sheria.

Imetolewa na:



Shaban A. Pazi

**KNY: KATIBU TAWALA WA MKOA
KILIMANJARO**

10/11/2019